# AckySHINE.com

# Mafundisho kuhusu Neema

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · February 28, 2017

Mafundisho ya Katekisimu · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Imani ya Kanisa Katoliki · #Katoliki: Kanisa Katoliki · #Katoliki: Mafundisho kuhusu Rehema na Neema · #Katoliki: Roho Mtakatifu

Je, tunaweza kuhakikisha neema ya utakaso?

Hapana, hatuwezi kuhakikisha neema ya utakaso kwa kuwa ni tukio ambalo linapita maumbile na kufanyika rohoni, hivyo halifikiwi na hisi zetu. Pengine Mungu anatokeza dalili fulani za badiliko hilo kama vile furaha ya ndani au karama ya nje, lakini hizo hazihitajiki wala hazitoshi kuthibitishia mtu amepata neema hiyo.

Neema ni nini?

Neema ni kipaji cha roho kinachopita nguvu za viumbe vyote; ndicho kipaji tupewacho na Roho Mtakatifu ili tupate uzima wa milele. (Lk 1:30, Rum 5:2)

Kuna aina ngapi za neema?

Kuna aina mbili za neema

1. Neema ya utakaso 2. Neema ya msaada

Neema ya Utakaso ni nini?

Neema ya Utakaso ni uzima wa Kimungu unaomiminwa na Roho Mtakatifu mioyoni mwetu. (Yoh 1:16, Yoh 3:3-5)

Neema ya Utakaso yapatikanaje?

Neema ya Utakaso yapatikana kwa; 1. Kwanza kwa Sakramenti ya Ubatizo 2. Sakramenti ya Kitubio 3. Kwa majuto kamili (majuto ya mapendo)

4. Yaongezwa kwa kupokea Sakramenti nyingine 5. Kwa Sala 6. Kwa Ibada Takatifu 7. Kwa matendo mema

Neema ya Utakaso yapoteaje?

Neema ya Utakaso yapotea kwa kutenda dhambi kubwa (dhambi ya mauti)

Kuna Faida ya kuwa na Neema ya Utakaso?

Faida ya kuwa na Neema ya Utakaso ni;-

1. Kupendwa na Mungu hapa duniani 2. Na kupokelewa kwake mbinguni baada ya kufa

Neema ya Msaada ni nini?

Neema ya Msaada ni msaada tupatao kwa Roho Mtakatifu kutuongezea nguvu Rohoni tutende mambo mema na tuepuke Mabaya

Neema ya Msaada yapatikanaje?

Neema ya Msaada yapatikana kwa kupokea Sakramenti, kusali, na kutenda mambo ya Ibada

(Yoh 15:5, 1Tim 2:4)